KISWAHILI
INSHA
MACHI-APRILI 2010
MUDA: SAA 1 ¾

KAMATI YA KUIMARISHA ELIMU
HATI YA KUHITIMU KISOMO CHA SEKONDARI (K.C.S.E)
MTIHANI TANGULIZI MWIGO

102/1
KISWAHILI
INSHA
MACHI-APRILI 2010
MUDA :SAA 1 ¾

<u>MAAGIZO:</u>

a) Andika insha mbili
b) Insha ya kwanza ni ya lazima
c) Changua insha nyingine moja kati ya zilizosalia
d) Kila insha hutuzwa alama 20
e) Insha zako zisipungue manaeno 400

1 Hivi karibuni elimu ya msingi bila malipo na elimu nafuu ya shule za upili imekabiliwa na changamoto nyingi.Umeteuliwa kama katibu wa tume ya kungunguza changamoto hizi na kuzipend ekeza kwa wizara ya elimu nchini.Andika ripoti hiyo.

2 Desturi ya viongozi kuoa wake wengi haifai.Jadili

3 Andika mtungo utakaofikiana na methali hii.Usione tangu la nguo ukasahau la miyaa"

4 Walipokaribia mtaa anakoishi Pamela ,kwa ghafla Pamela alipigwa pigo kubwa kwenye kisogo.Alipogeuka kutaka kujua ni nani aliyempiga kwa haraka alimwona yule mwanamume aliyetolea kumpeleka nyumbani akificha kitu ……….Endelea.

**KISWAHILI PAPER 2**

A UFAHAMU

Soma taarifa kasha fupisha kwa maswali yanayofuata.

Uwezo wa kuyakumbuka mambo ni hazina kuu kwa mtu yeyote yule aliye hai.Uwezo huu wa kukumbuka nimojawapo ya shughuli changamano za ubongo wa mwanadamuhutekeleza shughuli hii kwa namna tatu.Kwanza,ubongo hunasa jambo kasha huifadhi.Baadaye huanza mfumo wa kutoa kilichohifadhiwa ubongo ukiathirika kwa namna yoyote katika mojawapo ya njia hizi,basi uwezo wa kuyakumbuka mambo huvurugika.

Ingawa inaaminika kuwa uwezo wa kukumbuka hurithishwa toka kizazi kimoja hadi kingine,wataalamu wa masuala ya kiakili wanabaini kuwa uwezo huu unaweza kuimarishwa.Uimarishaji huu huhitaji mkakati madhubuti.

Njia mojawapo ya kustawisha uwezo wa kukumbuka ni kupitia kwa lishe.Vyakula vilivyosheheni vitamini B vyenye amino asidi Husaidia kuimarisha uwezo wa kukumbuka.Vyakula kama hivi ni mboga ,nyama(hasa maini),bidhaa za soya,matunda,maziwa,bidhaa za ngano ,samaki,pamoja na mayai.Vyakula vingine muhimu katika ustawihaji huu ni vile vyenye madini ya chuma.Madini ya chuma.Mdini haya huwezesha usambazaji wa hewa katika ubongo kwa wepesi .Vyakula ambayo vina madini haya ni mboga za kijani,mawele,ndengu,soya matunda kama maembe,ufuta(simsim),pamoja na nyama,hasa maini na mayai

Ubongo wa mwanadamu aliye hai hufanya kazi kila wakati awe macho au amelala.Utendaji kazi wake huendeshwa na glucose mwilini .Kwa hivyo vyakula vyenye sukari hii ni muhimu kuliwa.Hata hivyo lazima mtu awe mwangalifu na kuhakikisha kuwa mwili unakiwango cha sukari kisichohatarisha maisha.Haya yanawezekana kwa kula vyakula vyenye nyuzinyuzi kama vile mboga na matunda.

Njia ya pili ni kupiga marufuku vileo kama pombe na nikotini.Vileo hivi huathiri utaratibu wa kunasa,kuhifadhi na kutoa yaliyo ubongoni.

Iwapo mtu ana tatizo la kuyakumbuka majina ya watu,ni muhimu kufanya mazoezi ya kusikiliza kasha kurudia majina hayo wakati wa mazungumzo.Ni bora kulihusisha jina na sura na mtu.Kwa njia hii,ubongo utanasa na kuhusisha jina na kile kinacholengwa.

Woga wa kuvurugika kiakili ni mambo mengine tunayopaswa kuepuka kila wakati.Ni kawaida mtu kupata woga wakati anapokabili jambo asilokuwa na uhakika na matokeo yake kama mtihani au mahojiano.Lakinin anapaswa kuwa makini .Woga huo usikiuke mpaka na kumvuruga kiakili.Vurugu hizi huathiri kilichohifadhiwa ubongoni na pia namna ya kukitoa.

Hali kathalika,mwili wenye siha nzuri huhakikisha kuwa ubongo ni timamu .Wataalamu wengi wa siha wanakubali kuwa mazoezi ya kunyoosha viungo hustawisha ubongo na hivyo kuhakikisha kuweko kwa uwezo wa kukumbuka mambo.Ni muhimu kuwa na ratiba ya kunyoosha viungo kila wakati.Fauka ya hayo,Mazoezi ya kiakili ,kama vile kusoma ,akala yanayovutia,kujaza mraba na michezo mingine kama mafumbo,vitanza ndimi ni muhimu katika kustawisha uwezo wa kukumbuka.

Jamii ya watu wenye uwezo wa kuyakumbuka mambo ni jamii iliyopiga hatua kimaendeleo .Ni jukuma la kila mmoja wetu kuimarisha uwezo wa kukumbuka kila wakati.

Maswali Ufahamu

1 Ipe taarifa hii kichwa mwafaka________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

2 Taja mambo matatu yanayoweza kufanya ubongo kupoteza uwezo wa kuyakumbuka mambo.________________________________________________________________

________________________________________________________________________

______________________________________________________________________

________________________________________________________________________

_______________________________________________________________

3 Fafanua mambo yanayosababisha kutostawisha kwa uwezo wa kukumbuka (Al 4

4 Kwa kutoa mfano fafanua mbinu moja ya lugha iliyotumika katika ufahamu. (al 4)

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

_______________________________________________________________________

5 Eleza maana ya maneno yafuatayo.

i)Glukosi________________________________________________________________

_________________________________________________________________

ii) Siha

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

iii) Mfumo

________________________________________________________________________

_____________________________________________________________________

iv)Ratiba

________________________________________________________________________

______________________________________________________________________

v)Changamano

SEHEMU B UFUPISHO.

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali ya ufupisho.(Al.15)

Kuna mambo kadha ambayo yamejitokeza hivi majuzi yanayonitia wahaka kuhusu kuunda katiba ya aushi nay a kudumu.Mosi,kuna watu ambao wanachukulia kuwa lazima tuunde katiba itakayo Linda maslahi ya wanasisasa walioko sasa .Katika uundaji wa afisi mbalimbali wanafikiria maslahi ya watu wa makabila yao wala si asasi zinazohusika.Fikra hizi ndizo zilizowafanya watu kuandamana mitaani,wakiwahimiza wajumbe huhakikisha kuwa tuna afisi maalum zilizotengwa watu Fulani.Licha ya heshima tuliyo nayo kwa viongozi wetu wa sasa,si si sawa kuunda afisi kwa ajili yao.Tuunde afisi kwa sababu zinahitajika kwa maendeleo ya nchi yetu na zinalinda maslahi kila mwananchi.Tujitahidi kupunguza imani za kikabila katika kuunda sharia hii kuu.Tuongozwe na fikra za kizalendo:fikra za kujenga taifa moja kupitia lugha ya Kiswahili.

Pili ,kuna watu ambao kutokana na shinikizoza mataifa ya nje,wanataka tuwe na katiba itakayolinda haki za wageni kuliko za wananchi.Jambo hilo linasikitisha sana.Sheria hii kuu ni mali ya wakenya na ndio wanaopaswa kuiongoza na kuifikisha hatima yake.Kama ijulikanavyo na wengi.Katiba ni nyenzo ya kuleta maendeleo na kudumisha maelewano baina ya viongozi na wananchi.Ni mkataba baina ya mwanainchi mmoja na wenziwe kuhusu namna watakavyo ishi pamoja.Masharti yanayo iongoza serikali ni muhimu yawe kwa manufaa ya mwananchi; hayapaswi kukinzana na haki za mwananchi.

Katiba nyingi za ulimwengu zina kitangulizi kinachoonyesha kwamba katiba ni mali ya taifa na ndiyo sharia kuu nchini.Aidha,huonyesha kuwa wananchi wameafikiana kuwa ndiyo katiba yao na kwamba kuna masharti na maadili ya kimsingi yanayoiongoza.Kwa mfano ni nchi ya kidemokrasia ?Ni nchi iliyopunguza na kusambaza madaraka mashinani?Je,inaaminika katika heshima,usawa na haki kwa wananchi wote?Kuna imani yoyote kuhusu uraia,wimbo wa taifa,lugha za taifa?

Kitangulizi cha katiba ni mwongozo wa falsafa ya taifa na kinaashiria maafikiano baina ya wananchi kuhusu falsafa hiyo.Wanasiasa wanaochukua hatamu za uongozi wa serikali watatarajiwa kufuata imani na maelekezo ya kitangulizi hicho cha katiba.

Maswali:

a) Eleza jinsi ubinafsi na ukosefu wa fikra za kizalendo unavyohatarisha uundaji wa katiba ya aushi.
(maneno 30)

Nakala chafu

Nakala safi

b) Katiba ya wananchi inapaswa kushughulikia masuala yapi ya kimsingi? (maneno 25) (Alama 8)

Nakala chafu

Nakala safi

MATUMIZIYA LUGHA

a) Taja sauti mbili ambazo ni irabu na pia konsonanti (Al 1)

______________________________________________________________

b) Taja na ueleze aina za nomino katika sentensi hii.
Aliadhibiwa na kaumu alipokuwa kwenye mji. (Al 2)

______________________________________________________________

______________________________________________________________

(c) Tunga sentensi sahihi ukitumia nomino zifuatazo na kivumishi –enye (Al 2)

Kiroboto______________________________________________________

______________________________________________________________

Ndimi_________________________________________________________

______________________________________________________________

d) Eleza dhana zinazoonyesha viambishi awali katika kitenzi hiki HATUA KUCHEZEA (Al 2)

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

e)Tulikuwa watu watatu wanaume wawlil na mwanamke mmoja,(akifisha) (Al 2)

______________________________________________________________

______________________________________________________________

F) Andika katika wakati ujao hali timilifu. (Al 2)

______________________________________________________________

______________________________________________________________

g) Andika sentensi ifuatayo katika ukubwa na kasha udogo.
Mtoto wa mzee yule aligongwa na nyundo alipofukuzwa na mbwa. (al 4)

Ukubwa:

______________________________________________________________

______________________________________________________________

Udogo:

______________________________________________________________

______________________________________________________________

_____________________________________-

h)Unda vitenzi kutokana na nomino.

i) Ufisadi

______________________________________________________________________________
______________________________________________________________
ii) Mkwezi
______________________________________________________________________________
____________________________________________________________________________

i) Andika sentensi hizi ukifuata mnyambuliko uliomo mabanoni. (al 4)
a) Watoto waliji________________________ kwa uoga ( Kunja,kutendata)
ii) Mgonjwa huyu ana______________________ dawa kwa urahisi
(__________pa,fanyika)

J) Tumia 'O' rejeshi tamati katika sentensi zifuatazo:
i) Ubaguzi ambao alifanyiwa ulitutia aibu.
______________________________________________________________________________
______________________________________________________________________________
ii) Elimu ambayo ilifanyiwa ulitutia aibu.
______________________________________________________________________________
_____________________________________________________________________-

k) Ainisha kwa njia ya jedwali
Mtoto mtukutu ameadhibiwa na mwalimu mkuu.
______________________________________________________________________________
______________________________________________________________________________
______________________________________________________________________________
______________________________________________________________________________
_____________________________________________________________________________

Eleza moja kwa moja hadi shuleni kwa kutoka kumwona mwalimu (al 2)
______________________________________________________________________________
______________________________________________________________________________
______________________________________________________________________________
______________________________________________________________________________
_________________________________________________________________

m) Tunga sentensi ukionyesha matumizi ya neon huku kama: (AL 3)
i) Kivumishi
ii) Kielezi
iii) Kiwakilishi
______________________________________________________________________________
______________________________________________________________________________
______________________________________________________________________________
______________________________________________________________________________
______________________________________________________________________________

n) Yakinisha sentensi ifuatayo. (al 1)

i) mama hali wala hazungumzi.

o) Andika kwa wingi (al 1)
Pahali hapa ni pake.

p) Onyesha shamirisho kipozi na shamrisho kitondo katika sentensi hii. (al 2)
Mtangazaji aliwasomea habari watazamaji katika runinga.

q)Eleza maana mbili tofauti katika sentensi hii. (al2)
Aliletewa ng'ombe na motto wake.

r) Andika sentensi ifuatayo katika usemi halisi (al 2)
Kiptoo alisema kuwa angesafiri kwenda flax siku hiyo alasir.

D.ISIMU JAMII

(I) Eleza sifa za matumizi ya lugha katika rejesta ya maabadani. (alama 5)

(ii) Fafanua umuhimu wa lugha ya Kiswahili nchini Kenya. (alama 5)

**KISWAHILI PAPER 3**

1.(a) .Hapo kale,fasihi simulizi ilihifadhiwa vipi? (al 2)
(b) .Uhifadhi wa aina hiyo ulikuwa na udhaifu gain? (al 6)
(c) .Eleza vile fasihi simulizi anavyohifadhiwa siku hizi. (al 6)
(d) .Taja njia tatu za kukusanya fasihi simulizi. (al 3)
(e) .Njia za kisasa za kuhifadhi fasihi simulizi zina udhaifu gani? (al 3)

<u>KIFO KISIMANI</u>

Jibu swali la 2au la 3

2 Ndoto zimekifanya kichwa changu uwanja wa kuchezea .Karibu kila siku zinakuja kunipigia makelele .Mwangwi wa ndoto ya jana bado unavuma kichwani?

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 5)
b) Ni mbinu zipi za kisanaa zinazojitokeza katika nukuu hii? (alama5)
c) Eleza ndoto ya msemaji. (Alama 6)
d) Ndoto hii ni utabiri,eleza (Alama 4)

3 " Maisha bora ni viongozi" Thibitisha kauli hii ukirejelea tamthilia ya kifo kisimani (alama 20)

<u>UTENGANO</u>

Jibu swali la 4 au la 5

4 Eleza huku ukitumia mifano mbinu za kimyindo zifuatazo zinavyotumiwa katika riwaya ya utengano

(a) sadfa. (alama 8)
(b) Mjazi (alama 12)

5.'Lipi tena unalolitaka kwangu?ikiwa ni mapenzi unayasagasaga"
Maswali

(a) Eleza muktadha wa dondoo hii. (alama 4)
(b) Ni vipi msemewa alivyosagasaga mapenzi? (alama4)
(c) Taja na ueleze sifa za msemewa na msemaji katika muktadha huu/ (alama 12)

<u>6 MAYAI WAZIRI WA MARADHI</u>

'Fumbo la mwana'

'Ah……… na hata tabia na mienendo yenyewe nitaionea wapi nalini mwalimu?'

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
b) Onyesha vile ambavyo motto anayezungumziwa alivyobadilika (alama 10)
c) Taja na ueleze matatizo yanayowakabili watoto katika jamii hii. (alama 6)

USHAIRI

Soma shairi lifuatalo kasha ujibu maswali iliyopewa.

1 Simuoni mkulima mwenye uti wa uhai
Simuoni kusimama ,akaitetea rai
Mtima umemzima ,maisha ameburai
Amebaki nani?

2 Simwoni mtandakazi ,aliakimwaya jasho
Simwoni mwokozi,mleta udhibitisho
Kazama kapiga mbizi isiyokuwa na mwisho
Amebaki nani?

3 Simwoni na mwalimu mwenye sifa kamilifu
Aitowaye kaumu kizani kwa hitilafu
Sasa kawa kafahamu imevunja sharafu
Amebaki nani?

4 Simwoni daktari mtibu wa matibabu
Mwegema kwenye hatari mtoa katika tabu
Hakika amehajiri walobaki matibabu
Amebaki nani?

5 Simuoni na karani ajuaye kuratibu
Anayetia saini bila hofu kuharibu
Kazama kazama chini msemaji kawa bubu
Amebaki nani?

5 Simuoni na mwanazuo anyetoa mawazo
Falsafa za kileo na za juzi zipitazo
Hao wamepigwa ngeo na makubwa mangamizo
Amebaki nani?

7 Siwaoni wadilifu mashekha na makukhani
Ambao walisadifu kubashiri dunia
Sura zao badilifuwanafika mdomoni
Amebaki nani?

8 Siwaoni wa vyuoni walokuwa watukutu
Wanaotambua ya ndani nay a nje ya wenzetu
Wameishia gizani bongo zimejaa kutu
Amebaki nani?

9 Na wale wakali wasohofu mabishano
Wenye sifa kuhimili,hata uwe mvutano
Wanaukana ukweli wakati wa walekeano

Amebaki nani/

10 Naona kipya kizazi kimezaliwa yakini
Uwe wetu uombezi siku zijazo usoni
Wakati mtendaji lini itakuwa lini?
Umebaki nini?

Maswali

a) Eleza kikamilifu maudhui ya shairi hili. (al 5)
b) Eleza umbo la ubeti wa kwanza. (al 4)
c) Onyesha mbinu ya inkisari ilivyotumiwa katika shairi hili (al 2)
d) Andika ubeti wa tisa kwa lugha ya nathari. (al 4)
e) Mshairi ametoa ujumbe gain katika ubeti wa mwisho (al 2)
f) Eleza maana ya maneno haya jinsi yametumika. (al 2)

    i) Waadilifu
    ii) Walekeano

g) Taja tamathali iliyotumiwa katika kibwagizo. (al 1)